# Zaburi 89 - Ee Bwana, umekuwa kimbilio letu

**Siku ya Mungu ya 18, mwaka C**

Mus.: Jean-Claude BISIMWA
Harm.: Eugène AMPIRE Bisimwa




1. Unawaamuru watu warudi uvumbini,
   Ukisema: "Rudini, enyi wanadamu".
   Maana miaka elfu machoni pako / ni kama siku ya jana iliyopita,
   Na kama kesha la usiku.

2. Unawaondoa: wakawa kama ndoto asubuhi,
   Kama majani yanayomea:
   Asubuhi yana maua na kuwa mabichi,
   Jioni yanakatwa na kukauka.

3. Utufundishe kuzihesabu siku zetu,
   Tujipatie moyo wenye hekima.
   Urudi, ee Bwana: Mpaka wakati gani?
   Uwahurumie watumishi wako?

4. Utushibishe upesi kwa huruma yako,
   Nasi tutashangilia na kufurahi siku zetu zote.
   Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu;
   Na kazi ya mikono yetu utusitawishie.